

# Sera ya Bodi S-10: Karo za Wanafunzi na Misamaha ya Karo



## MAREJE

[Taratibu za Kiutawala kwa Sera ya Bodi S-10](#)

[Utah Code Ann. §53G-8-212, Kuharibu au Kutia Dosari Mali ya Shule – Wajibu wa Mwanafunzi](#)

[Utah Code Ann. §§53G-7-503-505, Karo, Amana, na Tozo za Wanafunzi](#)

[Utah Admin. Code R277-407, Karo za Shule](#)

## SERA

Bodi ya Elimu ya Wilaya ya Shule za Salt Lake City inahakikisha kwamba elimu bure inatolewa kwa wanafunzi wote wa wilaya kuanzia chekechea hadi darasa la 6. Kwa wanafunzi wa gredi 7-12, bodi inatambua hitaji la karo za wanafunzi ili kudhamini programu fulani za shule, shughuli za shule, na kozi, lakini imeahidi kupunguza mzigo wa kifedha wa karo za wanafunzi kwa familia. Pale karo ya shule inapotozwa, nia husika ni kuzisaidia shule kurejesha gharama bila ya kutengeneza faida yoyote. Kila juhudhi itafanywa ili kubakiza karo za wanafunzi kuwa ndogo kabisa. Kila mwaka, umma una fursa mbili za kutoa maoni kuhusu orodha ya karo inayopendekezwa kabla ya kuidhinishwa na kuitishwa na bodi. Wilaya itapitisha na kutekeleza karo, msamaha wa karo, na taratibu za kurudishiwa pesa kulingana na sheria za jimbo na sera hii.

Kusudi la sera hii ni kuhusu uanzishwaji sahihi wa mfumo mzuri wa karo, kutoa ilani ya kila mwaka kwa wanafunzi na wazazi/walezi wao kuhusu orodha ya karo iliyoidhinishwa na bodi na taratibu za msamaha wa karo, na kubainisha utendaji utakaowatenganisha wanafunzi wasiopeza kulipa wasishiriki katika shughuli zinazodhaminiwa na shule au kuwa mzigo kwa mwanafunzi au familia kiasi cha kwua na athari kubwa katika ushiriki.

Wilaya itatoa michakato yake mahsus kwa ajili ya utekelezaji wa sera hii ya bodi kuitia ambatanisho hili [taratibu za kiutawala](#).

S-10-Policy\_SWAHILI 2020-6-9

Hakuna mwajiriwa au mwanafunzi wa wilaya atakayebaguliwa katika ajira au programu au shughuli yoyote ya wilaya kwa misingi ya umri, rangi, ulemavu, jinsia, taarifa za vinasaba, utaifa, ujauzito, mbari, dini, utambulisho wa kingono, au hali ya ustaafu. Wilaya imedhamiria kutoa ufikio sawa na fursa sawa katika programu zake, huduma na ajira ikiwemo sera zake, michakato ya malalamiko, ufikiaji wa programu, matumizi ya huduma za wilaya, malazi na masuala mengine ya Fursa Sawa za Ajira. Wilaya pia inatoa ufikio sawa kwa huduma za wilaya kwa makundi yote ya vijana yaliyoorodheshwa katika Title 36 ya Sheria ya Marekani, ikiwemo makundi ya skauti. Mtu afuataye amechaguliwa kushughulikia maulizo na malalamiko kuhusiana na masuala ya ubaguzi, unyanysaj, na ulipizi ulio kinyume na sheria: Tina Hatch, Utii na Uchunguzi, 440 East 100 South, Salt Lake City, Utah 84111, (801) 578-8388. Unaweza pia kuwasiliana na Ofisi ya Haki za Kiraia, Denver, CO, (303) 844-5695.